

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:2460117
Fax: 255 - 022 – 2460117
e-mail: info@psc.go.tz;
Secretary@psc.go.tz;
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UBUNGO PLAZA,
BARABARA YA MOROGORO,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**WAAJIRI, MAMLAKA ZA AJIRA NA NIDHAMU KUWASILISHA
TAARIFA ZA KIUTUMISHI TUME YA UTUMISHI WA UMMA.**

Tume ya Utumishi wa Umma, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002 Kifungu cha 10(2), imepewa Mamlaka ya kuwataka Waajiri na Taasisi mbalimbali za Umma kuwasilisha taarifa zinazohusu masuala ya uendeshaji wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya kuonyesha Hali ya Utumishi wa Umma Nchini na kiwango cha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia masuala ya Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

Maeneo yanayotakiwa kutolewa taarifa kwa mujibu wa Mwongozo wa kuwasilisha taarifa wa Tume ni: **Masuala ya Ajira** (Ajira mpya; Kuthibitishwa kazini; Kupandishwa vyeo; Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi "OPRAS" na Mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya kuwajengea uwezo Watumishi).

Masuala mengine ni yale yanayohusu Nidhamu (Watumishi waliofukuzwa kazi; Watumishi waliopewa onyo; Kupunguzwa mshahara; Kushushwa cheo na Watumishi wenye kesi Mahakamani).

Pamoja na kwamba utoaji wa taarifa za Rasilimali watu **ni wajibu wa kisheria** ambao kila Mwajiri, Mamlaka ya Ajira na Nidhamu inapaswa kuutekeleza, bado hali ya uwasilishaji wa Taarifa hizi Tume siyo ya kuridhisha. Taasisi nyingi za Umma hazitekelezi ipasavyo jukumu hili la kisheria na baadhi ya Taasisi zinazotekeleza haziwasilishi taarifa zao kwa wakati.

Katika Robo ya Pili na ya Tatu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 uwasilishaji wa taarifa hizo ulikuwa **chini ya asilimia 30**. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Robo ya Pili ya mwaka wa fedha 2016/2017 ni Taasisi **120** tu kati ya **430** zilizopaswa kuwasilisha taarifa Tume, sawa na asilimia **27.9**, ndizo zilizowasilisha taarifa hizo. Taasisi **310** sawa na asilimia **72** hazikuwasilisha taarifa zao.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2016, ni Wizara **15** kati **19** ziliwasilisha sawa na asilimia **78.9**; Sekretarieti za Mikoa **10** kati ya **26** sawa na asilimia **38**; Wakala za Serikali **18** kati ya **37** sawa na asilimia **48.6**. Taasisi nyingine zilizowasilisha ni Idara Zinazojitegemea **10** kati ya **20** sawa na asilimia **50**; Taasisi za Umma **3** kati ya **143** sawa na asilimia **2** na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizowasilisha taarifa ni **69** kati ya **185** sawa na asilimia **37.3**.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2017, ni Wizara **6** kati **19** ziliwasilisha sawa na asilimia **32**; Sekretarieti za Mikoa **8** kati ya **26** sawa na asilimia **31**; Wakala za Serikali **16** kati ya **37** sawa na asilimia **44**. Taasisi nyingine zilizowasilisha ni Idara Zinazojitegemea **8** kati ya **2** | TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI 08/09/2017

21 sawa na asilimia **38**; Taasisi za Umma **2** kati ya **143** sawa na asilimia **2** na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizowasilisha taarifa ni **61** kati ya **185** sawa na asilimia **33**.

Takwimu hizi hazitoshi kuonyesha hali halisi ya utekelezaji wa masuala ya usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma Nchini kama unaendeshwa kwa misingi ya Sheria, Kanuni na Taratibu.

Tume inaendelea kusisitiza kuwa **"Uwasilishaji wa taarifa za Rasilimali watu ni jukumu la kisheria ambalo Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu"** zote zinapaswa kulitekeleza kwa wakati na kwa kuzingatia Mwongozo uliotolewa.

Tume inaziagiza Taasisi za Umma ambazo hazijawasilisha taarifa zao kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 kuhakikisha kuwa zinawasilisha taarifa hizo mapema ili kuwezesha kuandaa taarifa ya mwaka yenye kuonyesha hali halisi ya usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

Imetolewa na:



NYAKIMURA M. MUHOJI
KATIBU,
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
08 SEPTEMBER, 2017